



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA



**Unapojibu tafadhali taja:**

Kumb. Na . HBW:20/77/51

19 Disemba 2024

**TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE**

2. Halmashauri ya Wilaya ya Bunda imepokea mgao wa fedha kiasi cha Tsh. 350,000,000/= kutoka Wizara ya Fedha (Hazina) ikiwa ni mpango wa Serikali katika kuboresha maisha ya Watumishi wa Umma, Mikopo hii ni maalumu kwaajili ya ununuzi wa Magari, Samani, Pikipiki na Matengenezo ya vyombo vya Usafiri.

3. Watumishi wote wenye sifa mnakaribishwa kutuma maombi kwaajili ya mkopo tajwa kwa masharti yafuatayo;

- i. Mkopo huu utatolewa kwa Mtumishi mwenye Ajira ya Masharti ya Kudumu.
- ii. Mkopo utatolewa kwa Mtumishi aliyethibitishwa kazini.
- iii. Mkopaji (Mtumishi) anatakiwa kubakiwa na theluthi moja 1/3 ya mshahara wake baada ya makato ambayo atarejesha kwa kipindi kisichozidi miezi 72 (Miaka 6).
- iv. Mkopaji atatakiwa kulipa "Service charge" 3% na "Protect fund" 1% kutoka kwenye mkopo atakaokopa.
- v. Mkopo huu haununui deni kutoka Taasisi nyingine za Fedha na mwombaji ambaye tayari ana mkopo huu hatoruhusiwa kuongeza mkopo mwingine (top-up).
- vi. Mkopo unaotolewa kwa Mtumishi hauna riba.
- vii. Mkopo huu utatolewa kwa Mtumishi mwenye mwenendo mzuri kazini na utendaji mzuri wa kazi, aliyejaza na kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS) na ambaye hana mashauri ya kinidhamu.
- viii. Mwisho wa kutuma maombi haya ni tarehe **23/12/2024** saa **9:30** Alasiri.

4. **Maelekezo ya kufuata kwa Mkopaji.**

Mkopo huu utaombwa kwa njia ya mtandao (*internet*) kwa kufuata njia zifuatazo:-

- Ingiza link ya kuomba mkopo ambayo ni [als.muse.go.tz](https://als.muse.go.tz)
- Nenda sehemu ya *Register* ambapo utaingiza taarifa zako zote za Kiutumishi kama zinavyosomeka kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (e-Watumishi).

- Nenda sehemu ya *Verify Details* ambapo utatumiwa *Password* kwenye email yako binafsi.
- Nenda sehemu ya *username* ambapo utaweka *check number* yako na utaweka *password* yako kama ulivyotumiwa kwenye email yako.
- Ukishaingiza *password* uta *login* ambapo utapewa nafasi ya kubadili *password* au kuendelea na *password* uliyotumiwa.
- Utafungua mfumo na kuingia sehemu ya *Advance Loan*.
- Utakwenda moja kwa moja hadi sehemu ya *Apply Loan*.
- Utajaza taarifa zako za mkopo na mwisho utakwenda sehemu ya *Submit*.
- Baada ya hapo utasubiri maelekezo mengine kutoka kwa mwajiri kama utakuwa umekidhi sifa na utakuwa umepitishwa na Kamati ya Mikopo ya Halmashauri.
- Kwa usaidizi zaidi mwombaji atawasiliana na Afisa Utumishi kwa namba 0735-290-196 / 0755-402-543.

**NB:- Taarifa za mwombaji ambaye zitatofautiana na zilizopo kwenye Mfumo wa e-Watumishi basi Mtumishi huyo hatopata huduma ya kuomba mkopo wa Serikali kwa kuwa hatoweza kujisajili.**

### VIWANGO VYA MIKOPO

Aina ya Mkopo	Ngazi ya Mshahara	Kiwango cha juu cha Mkopo	Muda wa Marejesho
Mkopo Taslimu kwaajili ya Ununuzi wa Magari, Pikipiki, Samani na Matengenezo ya vyombo vya Usafiri.	TGS A-C TGTS A-C TGHS A-C TGOS A-C TGHOS A-C	Milioni 15,000,000/=	Miezi 72 (Miaka 6)
	TGS D-F TGTS D-F TGHS D-F	Milioni 30,000,000/=	Miezi 72 (Miaka 6)
	TGS G-H TGTS G-H TGHS G-H	Milioni 40,000,000/=	Miezi 72 (Miaka 6)
	LSSE 1-4 TGTS I TGHS I-J	Milioni 50,000,000/=	Miezi 72 (Miaka 6)

  
 Noel Micka Shamazugu  
 Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)  
 BUNDA.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
 HALMASHAURI YA MLLAYA YA BUNDA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), S.L.P 126, Bunda-Mara, Simu: Namba 028 2621055, Fax Namba: 0282621264, tovuti: [www.bundadc.go.tz](http://www.bundadc.go.tz), Barua Pepe: [ded@bundc.go.tz](mailto:ded@bundc.go.tz)